

Mazungumzo na Alan kuhusu Makala ya Imani



Tuambie kuhusu wewe mwenyewe.

Nina umri wa miaka minane. Nitakapokuwa nimekua, nataka kuwa mwansasansi maarufu. Rangi niipendayo ni rangi ya chungwa, na chakula nikipendeleacho ni *tortillas de patatas* (omeleti ya Kihispania) upishi wa bibi yangu.



VIELEZO NA TOBY NEWSOME

Je, ulijifunzaje Makala ya Imani?

Nilianza kujifunza katika darasa la Watoto. Tuliimba nyimbo ili kutusaidia kuzikariri. Nyakati zingine walimu wetu walizandika ubaoni na kufuta baadhi ya maneno. Pia tulichora picha ili kuelezea kile ambacho kila Makala ya Imani ilimaanisha.

Pia tulifanya mazoezi kuzisema pamoja na familia yangu ndani ya gari tukiwa njiani kwenda shule. Ninamsaidia dada yangu mdogo, Maia, kujifunza hizo pia. Naye pia anazijua sita za mwanzo!



Ni Makala ya imani ipi uipendayo?

Ninaipenda namba tisa. Tunaamini yale yote Mungu aliyoyafunua, na ambayo sasa anayafunua, na tunaamini kwamba bado Yeye atayafunua mambo mengi makuu na muhimu yahusuyo Ufalme wa Mungu. Inafundisha kwamba Baba wa Mbinguni anayo mambo mengi kwa ajili yetu kujifunza kidogo kidogo.



*Alan anatoka Málaga,
Hispania. Tulimuuliza
maswali kadhaa kuhusu jinsi
alivyojifunza Makala ya Imani.*

Ni kwa jinsi gani kuzijua Makala za Imani kumekusaidia wewe?

Siku moja shulen, rafiki yangu Sophia aliniuliza ninaamini katika nini na kama nilikuwa wa dini yoyote. Ninaikumbuka ile Makala ya Imani ya kwanza, ambayo inasema, "Tunaamini katika Mungu, Baba wa Milele, na katika Mwanae, Yesu Kristo, na katika Roho Mtakatifu." Hivyo nilishiriki hiyo pamoja naye.

Pia nilimwambia kwamba mimi ni Mkristo na muumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Alinisikiliza na kunielewa kile nilichoshiriki pamoja naye.



Je, uzoefu huu ulikufanya uhisi namna gani?

Nilihisi vizuri sana kwa sababu nilijuwa kuwa nimekuwa jasiri kushiriki imani yangu pamoja na rafiki yangu. Kwa sababu ya kufanya kwangu kazi kwa bidii kujifunza Makala za Imani, niliweza kushiriki injili na kujua nini cha kusema. ●